# JARIDA LA

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

*Wizara ya Furaha*

**Toleo la Mtandaoni: 09** | 12 Agosti, 2022 - TABORA | www.michezo.go.tz

## UMISSETA 2022 YAENDELEA KWA ARI YA USHINDANI



Wizara_SanaaTz

# UMISSETA 2022 YAENDELEA KWA ARI YA USHINDANI

12 Agosti, 2022



# Lindi na Dar es Salaam Zang'ara Kurusha Tufe UMISSETA 2022

Na Shamim Nyaki – **WUSM**

Mko wa Lindi umeibuka Bingwa katika mchezo wa kurusha Tufe upande wa Wasichana, kupitia mwanafunzi Mariam Serafin ambaye amerusha umbali wa Mita 8 Kwa Sentimita 98, huku Gift Kibanda kutoka Dar es Salaam akiubeba Mkoa wake kwa kurusha tufe umbali wa mita 10 kwa Sentimita 99.

Mchezo huo uliochezwa Agosti 12, 2022 Uwanja wa Sekondari ya Wavulana Tabora, ikiwa ni muendelezo wa Mashindano ya Michezo kwa Shule za Sekondari (UMISSETA) mwaka huu.

Katika mchezo huo upande wa Wasichana, namba mbili imechukuliwa na Mkoa wa Mtwara aliyerusha umbali wa mita 8 Kwa Sentimita 67, akifuatiwa na Marietha Msigwa kutoka Tanga ambaye amerusha mita 8 kwa Sentimita 60.

Kwa upande wa Wavulana, Mkoa wa Kigoma umekamata nafasi ya pili kupitia Ramadhan Tutu ambaye amerusha umbali wa mita 09 kwa Sentimita 89 akifuatiwa na Edward Michael kutoka Mkoa wa Dar es Salaam ambaye amerusha tufe umbali wa Mita 10 kwa Sentimita 85.

Mariam Serafini mshindi kutoka Mkoa wa Lindi, amesema siri ya kubeba ubingwa huo ni mazoezi na mbinu bora alizopewa na Kocha wake Tomas Wilson, pamoja na ari aliyokua nayo ya kuuheshimisha Mkoa wake, Huku Ramadhan Tutu wa Kigoma akisema sababu za ushindi ni kujituma, kufanya mazoezi pamoja na kusikiliza maelekezo ya Kocha vizuri.





**Mchezo wa Riadha umefanyika Agosti 12, 2022 katika Uwanja wa Tabora Wavulana, ukijumuisha mbio za mita 100 kwa Watu wa Makundi Maalumu, Mita 100 kwa Watu wa Kawaida pamoja na Mita 3000 Wasichana na Wavulana.**









406
118
828



# Tanga Yaanza Vizuri UMISSETA 2022

Na Bryson Mshana – **TABORA**

Mkoa wa Tanga umeanza vizuri katika michezo mbalimbali ya mashindano ya michezo kwa Shule za Sekondari 2022 (UMISSETA) iliyocheza hadi kufikia Agusti 11, 2022.

Mkoa wa Tanga haujapoteza mchezo wowote katika mashindano ya mwaka huu, huku timu za mpira wa Wavu, Kikapu, Netiboli na Miguu kwa Wasichana na wavulana zikiwa zimeshacheza.

Katika mchezo wa mpira wa miguu, wavulana Tanga ilianza kwa kutoshana nguvu na timu ngumi ya Mkoa wa Mwanza baada ya kutoka sare ya kufungana goli 1 – 1, mchezo ambao ulichezwa Agusti 10, 2022 mchana kwenye uwanja B Shule ya wavulana Tabora.

Mchezo huo ulikuwa wa kuvutia kwa dakika zote, na Tanga ilisawazisha goli kwa mkwaju wa penati kupitia kwa Sangu Ibrahim, baada ya kutanguliwa kufungwa mapema dakika ya 7 ya mchezo lililofungwa na Kelvin James wa Mwanza.

Mpira wa miguu Wasichana timu ya mkoa wa Tanga ilianza vizuri mashindano kwa kwa ushindi mnono wa magoli 4 – 0 dhidi ya Singida, katika mchezo ambao ulikuwa wa kuvutia kwa dakika zote.

Upande wa mpira wa Netiboli Tanga imeifunga Dodoma jumla ya magoli 26 – 18 kwenye mchezo uliochezwa Agosti 11, 2022 katika uwanja wa shule ya sekondari wasichana Tabora, huku Tanga pia ikitamba katika mchezo wa wavu kwa kuibuka na ushindi dhidi ya Mtwara.

Mkoa wa Tanga uliendeleza ushindi katika mchezo mpira wa kikapu wavulana ambapo kwenye mchezo wa awali uliibuka mshindi kwa kuifunga Songwe vikapu 72 – 16.



# Basketball Yapamba Moto UMISSETA 2022

Na Shamim Nyaki – **WUSM**

Mpira wa Kikapu kwa upande wa Wavulana unaendelea kwa ushindani mkali miongoni mwa mikoa inayoshindana mchezo huo, katika mashindano ya Michezo kwa Shule za Sekondari UMISSETA mwaka 2022 Tabora.

Katika michezo iliyochezwa Agosti 12, 2022 Viwanja vya Sekondari ya Wavulana Tabora, zimeshuhidiwa mechi kabambe zilizobeba vipaji vya hali ya juu kwa Wanafunzi, mechi kati ya Mkoa wa Pwani na Mwanza (Wavulana) umeshuhudiwa ukimalizikia kwa Mwanza kuibuka na ushindi wa magoli 27 kwa 25 ya Pwani.

Mkoa wa Singida umeichapa Tanga Magoli 44 Kwa 18, huku mchezo kati ya Tabora na Mbeya, Tabora wameibuka kidedea na ushindi wa magoli 29 kwa 28 ya Mbeya.

Katika mechi nyingine iliyokutanisha Mkoa wa Ruvuma na Katavi, Ruvuma imeicharaza Katavi magoli 39 kwa 09 , huku Kilimanjaro wakiikalisha Dodoma kwa magoli 31 kwa 25, kwa upande wa Dar es Salaam imeikalisha Kigoma kwa magoli 79 kwa 10.

Wanafunzi wakiwa wanachuana vikali katika Mchezo wa Mezani (Table Tennis) katika Mashindano ya Michezo kwa Shule za Sekondari yanayoendelea Agosti 12, 2022, Viwanja vya Sekondari ya Wavulana Tabora.





# Mpira Wa Miguu Wasichana, Mwanza Yaendeleza Ubabe UMISSETA

Na Bryson Mshana – **TABORA**

Timu ya soka ya wasichana kutoka Mkoa wa Mwanza, imeendelea kujizatiti kuwania Ubingwa wa UMISSETA 2022 baada ya kuibuka na ushindi wa goli 1 – 0 dhidi ya mkoa wa Mara.

Katika mchezo uliochezwa Agusti 12, 2022, uwanja wa ya Sekondari ya wavulana Tabora umeshuhudia Mwanza ikipata ushindi wa pili mfululizo baada ya ule wa 2 -0 ilioupata dhidi ya Kagera.

Kocha wa Mwanza Michael Oty amesema mchezo wao na Mara ulikuwa mgumu kutoka na umahiri wa wachezaji wa timu zote mbili na ushindi walioupata umedhihirisha ubora wa wachezaji wake.

Katika michezo mingine iliyochezwa Agusti 12, 2022 Singida iliifunga Ruvuma 4 – 0, na Dar es salaam kuibuka na ushindi wa 2 – 0 mbele ya Kilimanjaro iliyotoka kuishinda Ruvuma 3 – 1 kwenye mchezo wa ufunguzi.

Kwa upande wa Mkoa wa Songwe uliibuka na ushindi wa magoli 2 – 0 mbele ya Shinyanga, wakati Kagera ilifufua matumaini ya kusonga mbele baada ya kuishinda Katavi 2 – 1.

Mchezo mwingine wa kusisimua ulikuwa wa Morogoro na Geita, uliomalizika kwa Morogoro kuibuka mshindi kwa magoli 2 – 0 huku Manyara ikiishinda Mtwara 1 – 0 na Arusha na Njombe kutoshana nguvu kwa sare ya 2 – 2.

Mbeya iliibuka na ushindi mnono wa 3 – 0 dhidi ya Iringa, Dodoma ikaishinda Simiyu 3 -2 na wenyeji Tabora wakapata matokeo ya magoli 2 – 0 mbele ya Pwani iliyotoka kupoteza 7 – 0 kwa Dodoma kwenye mchezo wa ufunguzi.

# UMITASHUMTA | UMISSETA
# 2022

# #SensaBika

Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo